# Hadithi 35

# KURIDHIA MAKADIRIO

Kutoka kwa Abu Hurairah, amesema: amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na Amani ziwe juu yake) Tizameni walio chini yenu,

1 Na wala msitizame walio juu yenu

2 Kufanya hivyo ni sababu bora ya kuwafanya msizidharau neema za Mwenyezi Mungu kwenu[1]"

1 Muslim (2963).

## Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu

- *﴿Kwa hakika tumevifanya vilioko juu ya ardhi kuwa ni pambo lake ili tuwafanyie mtihani, ni nani kati yao wenye vitendo vizuri zaidi﴾ [kahfi: 7].*
- *﴿Wala usivikodolee macho tulivyo wastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao, kwa ajili ya mapambo ya duniani, ili tuwajaribu. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora na inadumu zaidi﴾ [Twaha: 131].*
- *﴿Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale walio kuwa wanataka maisha ya duniani: Laiti tungeli kuwa tunayo kama aliyo pewa Qaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa. 80. Na wakasema wale walio pewa ilimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipo kuwa wenye subira﴾ [Qaswas: 79, 80].*
- *﴿Kwani wao ndio wanao gawa rehema za Mola wako Mlezi? Sisi tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wenginewe wawatumikie. Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayo yakusanya﴾ [zikhruf: 32]*

## Msimulizi

Ni Abuu Hurairah, jina lake – kwa kauli yenye ngu – ni Abdur rahmaan bun Swakhar, ukoo wa Ad dausiy, kabila la Azdiy myemeni. Amezaliwa takribani miaka ishirini kabla Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) hajahamia Madina, kisha akasilimu mwaka wa Khaibar, mwaka wa 7H. ameishi na mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kwa ajili ya kutafuta elimu akilizika kwa kiasi kidogo cha chakula anachokipata, akahifadhi Hadithi za Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), akawa ndiye swahaba aliye hifadhi Hadithi nyingi. Alipewa uongozi kuiongoza Bahraini kwa muda, lakini muda wake mwingi alikuwa Madina. Amefariki akiwa Madina mwaka 58H[1].

## Muhtasari

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) ana amrisha maswahaba zake watizame walio chini yao kineema na mambo ya kiDunia, walio mafakiri na madhaifu zaidi yao, na wala wasitizame alio wafadhilisha kwa riziki, afya na neema za kiDunia, kufanya hivyo ni bora na inapelekea kutodharau neema za Mwenyezi Mungu.

1 Rejea yake ufafanuzi wake katika: "Maarifaat al-Sahaba" na Abu Nu'aym (4/1846), "aliastieab fi maerifat al'ashabi"na Ibn Abd al-Bar (4/1770), "Asad al-Ghaba" na Ibn al-Atheer (3/357), "Al-Isbah fi Tamazu al-Sahaba" cha Ibn Hajari Asqa-lani (4/267) .

# Ufahamu

1. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anahimiza maswahaba zake na umma wote watizame walio chini yao katika mambo ya kidunia, kama mali, sura na mfano wa hayo, kama mafakiri, wahitaji, madhaifu, wagonjwa, wenye mahitaji maalumu na wengine wengi, wataona jinsi Mwenyezi Mungu alivyowafadhilisha.

2. Na Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amezuia kutizama walio juu kidunia na wenye nguvu na afya njema, kama anavyosema Mwenyezi Mungu: "131. Wala usivikodolee macho tulivyowastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao, kwa ajili ya mapambo ya duniani, ili tuwajaribu. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora na inadumu zaidi. [Twaha: 131].



3 Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amebainisha sababu ya kufanya hivyo ni kupelekea wasidharau neema ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaneemesha. Mwanadamu akimtizama aliye chini yake kidunia, anatambua kwamba, Mwenyezi Mungu amemfadhilisha zaidi kuliko watu wengi, atalipokea hilo kwa shukurani, kutenda wema na kuilipa neema hiyo kwa kufanya ibada. Ama akitizama wenye neema na akijikita kutizama maisha yao ya kidunia na jinsi Mwenyezi Mungu alivyowaneemesha, na hilo likampelekea kujilinganisha nao, itampelekea kukufuru neema za Mwenyezi Mungu na huenda likampelekea katika husda na kinyongo. Hadithi haimaanishi kwamba, mja aache Dunia, na wala asifaidike kwa alichojaaliwa na Mwenyezi Mungu, bali makusudio asiruhusu Dunia kujikita katika moyo wake, kiasi kwamba haridhiki na alichojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.



# Mafunzo

1 Mwanadamu anaweza kuona au kusikia mtu ambae yuko vizuri kidunia, inatakiwa ajitibu mwenyewe kwa kutizama aliye chini yake, kama alivyosema Mtume Mtukufu.A: “anapo ona mmoja wenu aliye bora kimali na umbile, basi amtizame aliye chini yake”[1].

2 Inatakiwa muumini aweke akhera mbele ya macho yake, asitizame neema za Dunia, na wala asikithirishe kuwatizama waovu, kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaandalia waja wake wema katika Pepo: “mambo ambayo jicho alijawahi kuyaona, wala sikio kuyasikia, wala mwanadamu yeyote kuyawaza”[2], ikitoke jicho lake kutizama kitu chochote katika mapambo ya Dunia, basi asiipeleke nafsi yake huko, inatakiwa akumbuke neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ambazo amewaandalia waja wake wanaomuogopa.

3 Badili kipimo chako cha kutathmini mambo, na ukumbuke kwamba neema za uhakika, hadhi na za milele, ziko Peponi. Kwa kufanya hivyo, utabadili tabia ya ushindani katika mambo ya kidunia na kuwatamani waliopewa neema hizo. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amesema: “hakuna husda ila katika mambo mawili; mtu ambae Mwenyezi Mungu amemjalia mali, akalazimika kuitumia katika mambo ya kheri, na mtu ambaye Mwenyezi Mungu amemjaalia hekima anaitumia kutatua migogoro na kusomesha”[3].

4 Kaaroon alipovuka mipaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na akawa jeuri mwenye kiburi, kwa sababu ya neema alizojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, watu wanye nafsi dhaifu walimtizama kisha wakasema: (: Laiti tungelikuwa tunayo kama aliyopewa Qaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa.” [qaswas: 79]. hawakuhifadhi macho na nafsi zao zisifitinishwe kwa neema za kidunia alizojaaliwa, na wala hawakupata chochote katika neema hizo. Walikuwa kama alivyosema mshairi:

Umeona ambalo haulimudu***wala hauwezi kulivumilia walau kidogo.

5 Amesema Ibn a’wn -Mwenyezi Mungu amrehemu-: nimeishi na matajiri, nikaona matatizo yangu yana naafu kuliko yao, na nimeishi na mafukara nikajihisi nina raha[4].

6 Muumini anapo tambua kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amegawa riziki kwa hekima zake, nafsi yake inatulia, na wala hawazi vile alivyowajalia wengine zaidi yake katika neema za kidunia.

1 Al-Bukhari (6490) na Muslim (2963).

2 Al-Bukhari (3244) na Muslim (2824).

3 Al-Bukhari (73) na Muslim (816), kutoka kwa Ibn Masoud

4 “Tarth Al-Tathreeb fi Sharh Al-Taqreeb” cha Al-Iraqi (8/145, 146).

7 Katika mambo makubwa yenye kuleta furaha katika moyo wa muumini, ni kutambua neema nyingi za Mwenyezi Mungu Mtukufu alizomneemesha, na azitizame kwa jicho la mazingatio, na kutizama walio chini yake, kama alivyosema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: “mwenye kuamka asubuhi kati yenu akiwa na amani, na akiwa na afya katika mwili wake, na akiwa na chakula cha siku hiyo, basi huyo ni kama amepewa kheri za dunia nzima[1] ”

8 Mtu anapo pata mtihani au msiba, kutizama walio chini yake kunapelekea kuona kwamba yeye ana nafuu,. Hilo litamfanya awe mvumilivu na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa afya aliyo mjaalia.



**Amesema mshairi:**

*Shikamana na uchamungu na rizika kwa alicho kujalia Mwenyezi Mungu***mja bora wa Mwenyezi Mungu ni yule mwenye kurizika.*

*Usihangaike na Dunia wala usiwe na taama***tamaa zinaweza kumuangamiza anaye jidanganya kuzifikia.*

**Na amesema mshairi mwingie:**

*Niliona kurizika ni vazi la utajiri***nikawa nashikamana nalo.*

*Heshima yake ikanivisha vazi ***masiku yanaenda bila kudhalilishwa.*

*Nikawa tajiri bila hela***natembea nikiwa na heshimiwa kama mfalme.*

1 Al-Tirmidhiy (2346), kutoka kwa Ubayd Allah bin Muhswin.

